# MSWADA WA USHIRIKI WA UMMA, 2024

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu*

### SEHEMU I—UTANGULIZI

1. —Kichwa kifupi
2. —Ufafanuzi
3. — Lengo la Mswada

### SEHEMU II—USHIRIKI WA UMMA

4. — Upeo wa ushiriki wa umma.
5. — Uamuzi wa ofisi inayowajibika

### SEHEMU III—MIONGOZO YA JUMLA YA USHIRIKI WA UMMA

6. — Yatakayozingatiwa kwa ushiriki wa umma
7. —Taarifa
8. —Ufikiaji wa mchakato wa ushiriki wa umma
9. —Muda wa kutosha
10. —Kupata stakabadhi.
11. —Kutayarisha majibu
12. —Mwenendo katika jukwaa lla ushiriki wa umma

### SEHEMU IV—MIONGOZO MAALUM YA USHIRIKI WA UMMA

13. —Kutayarisha miongozo maalum ya ushiriki wa umma.
14. —Uchapishaji wa miongozo maalum
15. —Ushiriki wa bunge la Kitaifa.

### SEHEMU V—MASHARTI YA ZIADA

16. —Adhabu ya Jumla.
17. —Utoaji wa mpito

**MSWADA WA USHIRIKI WA UMMA, 2024**

**Mswada wa**

**SHERIA inayoangazia ushiriki wa umma;kuweka katika athari kanuni za Kikatiba,demokrasia na ushiriki wa Umma kwa mujibu wa vipengee vya 10(2), 69(1)(d), 118, 184(1)(c), 196, 201(a) na 232(1)(d vya Katiba na kusudi nyinginezo husika.**

**IMETUNGWA na bunge la Kenya, ifuatavyo-**

**SEHEMU I— UTANGULIZI**

Kichwa cha Habari.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ushiriki wa Umma,2024.

Ufafanuzi

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji maana nyingine, maneno yafuatayo yatapewa maana hizi-

"ofisi ya umma" ina maana iliyopewa katika kipengee cha 260 cha Katiba

"ofisi inayowajibika" ina maana ya ofisi itakayowajibika na maswala ya ushiriki wa umma katika taasisi zilizotajwa kwenye kifungu cha 6;

"chombo cha serikali" ina maana iliyopewa katika kipengee cha 260 cha Katiba; na

"miongozo maalum" ina maana ya miongozo ya ushiriki wa umma iliyotayarishwa na ofisi inayowajibika chini ya kifungu cha 7.

Lengo la Sheria.

**3.** Lengo la Sheria hii ni kuimarisha, kukuza na kuwezesha ushiriki wa Umma katika michakato ya Utawala na hasa yafuatayo-

(a) Kuipa uzito kanuni za ushiriki wa umma zilizoratibishwa kwenya vipengele

1(2),10(2), 69(1)(d), 118, 184(1)(c), 196, 201(a) na 232(1)(d) vya Katiba

(b) Kukuza demokrasia na ushiriki wa watu kama ilivyodokezewa katika kipengele cha 10 cha Katiba;

(c) Kukuza uwazi na uwajibikaji katika katika kufanya maamuzi; na

(d) Kuimarisha ufahamu wa umma na kukuza ushiriki wa umma katika michakato ya utawala.

## SEHEMU II — USHIRIKI WA UMMA

Upeo wa ushiriki wa umma

**4.** Idara ya Umma au ofisi ya umma itawezesha ushiriki wa umma katika maswala yafuatayo—

(a) uundaji wa sera;
(b) kupanga bajeti na usimamizi wa fedha;
(c) mchakato wa kutunga sheria;au
(d) jambo lingine lolote kama ilivyodokezwa kwenye sheria.

Uamuzi wa ofisi inayowajibika

**5.** Ofisi inayowajibika kwa mujibu wa Sheria hii itakuwa—

(a) Ikiwa ni bunge, kamati inayohusishwa na maswala yanayozingatiwa;
(b) Ikiwa ni idara ya mahakama, itakuwa Jaji Mkuu;
(c) Ikiwa ni wizara au idara ya serikali, itakuwa ni waziri wa wizara hiyo;
(d) Ikiwa ni Ofisi ya mwanasheria mkuu itakuwa mwanasheria Mkuu;
(e) Ikiwa ni Ofisi ya mkuu wa mashtaka, itakuwa ni mkuu wa mashtaka ya Umma;
(f) Ikiwa ni tume au ofisi ya kujitegemea, itakuwa ni katibu au kiongozi wa tume hiyo;

(g) Ikiwa ni bunge la kaunti, itakuwa kamati ya bunge la launti inayohusishwa na maswala yanayozingatiwa; na

(h) Ikiwa ni kamati kuu ya kaunti itakuwa mwakilishi wa kamati hiyo kuu ya kaunti.

## SEHEMU III—MIONGOZO YA JUMLA YA USHIRIKI WA UMMA

Mambo ya kuzingatia wakati wa ushiriki wa umma

**6.** Ofisi inayowajibika itazingatia yafuatayo inapofanya ushiriki wa umma—

(a) Aina ya jambo linalozingatiwa;

(b) Uharaka wa jambo hilo;

(c) Athari ya jambo hilo kwa umma;

(d) Hitaji la kujumuisha na uwakilishi wa ufanisi;

(e) Nambari ya watu watakaoathiriwa;

(f) Uwezo wa umma kupata habari inayostahili na jukwaa la ushiriki wa umma; na

(g) Uadili na uwazi wa mchakato huo.

Taarifa

**7.** (1) Ofisi inayowajibika itatoa taarifa kwa umma ili kuwapa muda wa kutoa maoni yao kwa jambo linalozingatiwa.

(2) kwa ajili ya ibara ndogo ya (1), ofisi inayowajibika itaweka mikakati itakayohakikisha kwamba uchapishaji wa taarifa itafikia watu wengi zaidi kupitia njia za—

(a) runinga;
(b) vituo vya teknolojia za habari;
(c) tovuti;
(d) redio za jamii;
(e) mikutano ya umma; au
(f) magazeti.

(3) programu ya ushiriki was umma katika ibara ndogo ya (1) itaweka wazi yafuatayo—

(a) Kusudi maalum ya mashauriano;
(b) jamii, taaluma au vikundi vitakavyotoa ushauri;
(c) urefu wa mashauriano;
(d) ikiwa mawasilisho yatafanywa kwa njia ya kuongea au kuandika au kwa njia zote mbili; na
(e) mambo yatakayozingatiwa katika mashauriano.

Ufikiaji wa mchakato wa ushiriki wa umma

**8.** (1) Ofisi inayowajibika itahakikisha kwamba umma inapata mchakato ambao ni wa haki na usawa na kupata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu mambo yanayozingatiwa.

**9.** Ofisi inayowajibika itazingatia hatua zinazofaa kuwezesha wanawake, walemavu, vijana, kabila zote na vikundi vya walio wachache na vikundi vilivyotengwa kujumuika katika ushiriki wa umma.

(3) ikiwa washiriki walengwa hawaelewi lugha za kitaifa, ofisi inayowajibika itahakikisha kuwa kuna utafsiri.

Muda wa kutosha

**10.** Ofisi inayowajibika itahakikisha kwamba kuna muda wa kutosha katika ushiriki wa umma.

Kupata stakabadhi

**11.** Idara inayowajibika itahakikisha kwamba stakabadhi zote za jambo linalozingatiwa zinapatikana.

Kutayarisha majibu

**12.** Ofisi inayowajibika itafanya yafuatayo—

(a) Itazingatia na kutilia maanani maoni yaliyotolewa na umma; na
(b) Kutoa sababu za uamuzi wa mwisho kwa umma

Mwenendo katika vikao vya ushiriki wa Umma

**13.** (1) Mtu atakayejumuika katika kikao cha ushiriki wa umma atafanya hivyo kwa heshima na kuzingatia wengine.

(2) Uhuru wa kujieleza uliodokezwa kwenye kipengele cha 33 cha katiba utatumiwa tu ili kuwezesha ushiriki wa umma chini ya ibara ndogo ya (1).

(3)Idara inayowajibika inaweza kuondoa mtu ambaye hawezi kufuata kanuni za ibara ndogo ya (1) katika kikao cha ushiriki wa umma.

## SEHEMU IV—MIONGOZO MAALUM YA USHIRIKI WA UMMA

Kutayarisha miongozo maalum ya ushiriki wa umma

**14.** (1) Ofisi inayowajibika itatayarisha miongozo maalum ya kutekeleza ushiriki wa umma.

(2)Miongozo maalum ya ushiriki wa umma itakayotayarishwa na ofisi inayowajibika itazingatia masharti katika sehemu ya III.

(3)Kila kitengo cha bunge kitazingatia miongozo ya ushiriki wa umma katika sheria za kudumu na kuhakikikisha kwamba sheria hizi zinapatikana kwa rahisi.

Kuchapisha kwa miongozo maalum ya ushiriki wa umma

**15.** (1) Ofisi inayowajibika itachapisha miongozo maalum ya ushiriki wa umma iliyotayarishwa kupitia ibara ya 14 kwenye gazeti la serikali.

(2) Masharti ya ibara ndogo ya (1) haitatumika kwenye bunge la Kitaifa au bunge za kaunti.

Ushiriki wa Umma katika bunge la kitaifa

**16.** (1) Kwa mujibu wa kipengee cha 118(1) cha Katiba, Bunge la Kitaifa litafanya yafuatayo—

(a) Kufanya mambo yake kwa njia ya uwazi, na vikao vyake na vya kamati zake vitawekwa wazi kwa umma.; na
(b) Kuwezesha ushiriki wa umma na kushirikisha bunge na kamati zingine za bunge.

(2) Ikiwa kamati ya kwanza ya Bunge la kitaifa itafanya ushiriki wa umma ya mswada, kamati ya pili ya bunge inaweza kufanya yafuatayo—

(a) Kutegemea ripoti iliyotolewa na kamati ya kwanza; au

(b) Kuhitaji maoni ya ziada kwa mswada kuhusu marekebisho yaliyofanywa kwenye mswada wakati inapozingatiwa;

(4) Kamati ya kitengo kimoja cha bunge inaweza kufanya ushiriki wa umma kwa pamoja na kamati nyingine yeyote ya kitengo cha pili cha bunge kuhusu mswada unaotoka kwenye chama cha kisiasa kinachotengeneza serikali kuu.

(5) Kamati ya kitengo cha pili cha bunge la kitaifa itachukua hatua ili kuhakikisha hakuna marudio ya ushiriki wa umma uliofanywa na kitengo cha kwanza cha bunge.

## SEHEMU V—SHERIA ZA ZIADA

Adhabu ya jumla

**17.** Mtu yeyote ambaye atakiuka sheria na masharti iliyotolewa katika sheria hii ana makosa na akipatikana na hatia-

(a) Ikiwa ni binadamu atalipa faini isiyopungua shilingi elfu mia tatu; na

(b) Ikiwa ni shirika italipa faini isiyopungua shilingi elfu mia tano.

Utoaji wa mpito.

**18.** Ikiwa zoezi la ushiriki wa umma linaendelea wakati wa kuanzishwa kwa sheria hii, zoezi hilo litaendelea lakini kwa kufanya hivyo, litatilia maanani sheria hii kwa kiasi kikubwa.